



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA, NA WENYE ULEMAVU

TAARIFA KWA UMMA

WITO KWA VYUO NA TAASISI ZA MAFUNZO KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUTOA MAFUNZO YA UANAGENZI KUANZIA SEPTEMBER, 2019 HADI JUNI, 2020

- 1.0. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini. Utekelezaji wa Programu hii umegawanyika katika sehemu kuu Nne (4) ambazo ni: Mafunzo ya Uanagenzi; Mafunzo ya kuongeza Ujuzi kwa Wafanyakazi; Mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wa vyuo; na Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa Mafunzo. Lengo kuu la mafunzo ni kusaidia vijana kuwa na Ujuzi wa kuwawezesha kushindana katika soko la ajira ndani na nje, kuongeza wigo mpana wa kujiajiri au kuajiriwa.
- 2.0. Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Waziri Mkuu imepanga kutoa mafunzo ya Uanagenzi kwa Vijana 17,000 katika Fani mbalimbali yakiwemo: mafunzo ya uashi, useremala, utengenezaji wa magari, ufundi bomba, ufundi umeme, uhomeleaji na uungaji vyuma, ubunifu wa Mitindo ya mavazi na ushonaji, Mapishi, uwekaji wa marumaru (terrazzo) na vigae, kutengeneza madirisha ya aluminium na P.V. C, ufundi wa Umeme na umeme wa Magari, ufundi wa viyoyozi vya magari, Ususi na urembo (beautification), utengenezaji viatu, utengenezaji simu, Radio, televisheni na Kompyuta, Uchanganyaji wa rangi, ufugaji wa samaki, uchimbaji na uongezaji thamani madini, na kuchakata mazao mbalimbali ikiwemo kahawa, korosho, ngozi n.k.
- 3.0. Mafunzo yatatolewa kwa vijana wa kitanzania wenye umri usiozidi miaka 35 na yatakuwa ya muda wa miezi Sita (6). Mafunzo yatafanyika katika mikoa yote nchini.

4.0. Sifa za Vyuo na Taasisi kushiriki kutoa Mafunzo:

- a) Vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) au Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) yenye Daraja A, B na C;
- b) Vyuo na taasisi zenye uwezo na kutoa mafunzo kwa fani husika kuanzia wanafunzi 100 na kuendelea;
- c) Vyuo vyenye Wakufunzi walioajiriwa na Chuo husika na wanatambulika na Serikali;
- d) Vyuo vyenye uwezo wa miundombinu ya kufundishia; na
- e) Vyuo vyenye uzoefu usiopungua miaka mitano (5) na vimetoa mafunzo husika mfululizo

5.0. Vyuo vyenye sifa za kutoa Mafunzo kwa mojawapo ya fani zilizoainishwa vinashauriwa kuomba kutoa Mafunzo husika kwa utaratibu ufuatao:

- a) Barua ya kuomba kutoa mafunzo ikianisha fani zitakazotolewa na idadi ya wanafunzi kwa fani;
- b) Sifa za wakufunzi watakaotoa mafunzo (CV);
- c) Muda wa kutoa mafunzo;
- d) Cheti cha usajili wa chuo;
- e) Cheti cha mlipa Kodi (Tax Identification Number);
- f) Gharama za kutoa mafunzo kwa fani na kwa mwanafunzi; na
- g) Maelezo mengine ya ziada kadiri itakavyofaa.

6.0. Vyuo na Taasisi zitakazo wasilisha maombi zitafanyiwa upekuzi kuona kama zina uwezo wa kutoa mafunzo husika. Vyuo na Taasisi zitakazokidhi vigezo zitaitwa kwa majadiliano na Serikali kuhusu namna bora ya kushirikiana kutoa mafunzo husika.

7.0. Vyuo na Taasisi zinazopenda kushiriki kutoa mafunzo viwasilishe maombi kwa Katibu wa Bodi ya Ununuzi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, **S. L. P. 2890, DODOMA, Mji wa Serikali, Mtumba, Mtaa wa Kazi**. Maombi yawasilishwe kabla ya tarehe 30 Julai, 2019 saa 9.00 Alasiri.

Imetolewa na:
KATIBU MKUU